

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

### WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI SERIKALINI (GPSA)

#### TANGAZO LA AJIRA YA MUDA YA MUHUDUMU WA PUMP ZA MAFUTA NAFASI MBILI (2)

06/08/2018

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997, kupitia katika Agizo la uanzishwaji wa Wakala "Establishment Order 2007" kwa Tangazo la Serikali Na. 235 la tarehe 7 Desemba, 2007. Aidha Agizo la uanzishwaji lilifanyiwa marekebisho tarehe 13 Aprili, 2012 kupitia Tangazo Na.133. Wakala ulizinduliwa rasmi tarehe 16 Juni, 2008 na una ofisi katika Mikoa yote ya Tanzania bara.

Mtendaji Mkuu wa Wakala (GPSA) anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi ya Muda ya Mhudumu wa Pump za Mafuta katika **Mkoa wa Dodoma**.

#### MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania
2. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
3. Maombi ya mwombaji yaambatane na nakala za vyeti vyote vinavyohitajika.
4. Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 35.
5. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi mhusika atachukuliwa hatua za kisheria.
6. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

## **KAZI: MUHUDUMU WA PUMP NAFASI MBILI (2)**

### **SIFA:**

#### **Mwombaji lazima ;**

- Awe amehitimu kidato cha Nne na ufaulu wa cheti chenye angalau D. mbili tu.

### **1. Majukumu**

Majukumu ya 'Muhudumu wa Pump' yatakuwa:

1. Kupima mafuta kwenye visima (dipping) kila siku asubuhi na jioni.
2. Kusoma Mita ya pump kila asubuhi.
3. Kutoa mafuta kwenye vyombo husika
4. Kujaza kitabu cha mauzo ya kila siku
5. Kuhakikisha usalama na ulinzi wa pump wakati wa matumizi.
6. Kutoa taarifa ya mauzo ya siku kupitia kitabu cha mauzo.
7. Kuandaa na kutoa taarifa ya mapokezi, mauzo na bakaa ya mafuta.

### **MAELEKEZO YA MTUMAJI MAOMBI**

Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa Meneja wa mkoa, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) S.L.P. 287 DODOMA . Mwisho wa kupokea maombi husika ni tarehe 12.08.2018. Aidha uchambuzi utafanyika na watakaoitwa kwenye usaili ni wale tu watakaokuwa wamekidhi vigezo husika.

Imetolewa na;-

MTENDAJI MKUU,

WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI SERIKALINI (GPSA),

S.L.P. 9150,

DAR ES SALAAM,

TANZANIA.